



DAWASA YETU

WIKI HII - TOLEO NA: 247

TAREHE: 21.10.2026 - 27.10.2026



MRADI KIMARA B WAFIKIA 80%, WAKAZI 30,000 KUNUFAIKA



Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (**DAWASA**) Mkoa wa Kihuduma Ubungo inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi **30,000** kupitia utekelezaji wa mradi wa uboreshaji huduma wa **Temboni** hadi **Mkwajuni**.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Msimamizi wa Miradi **DAWASA Ubungo**, Mhandisi **Dorcas Shabani**, amesema mradi huu ni sehemu ya jitihada za Mamlaka za kuhakikisha wakazi wa **Kimara B** wanapata huduma ya majisafi kwa uhakika zaidi.

"Mamlaka imejidhatiti kuhakikisha huduma ya maji kwa wananchi wa **Kimara Temboni** hadi Mkwajuni inakuwa nzuri na ya uhakika, kwa kutekeleza mradi huu kwa fedha za ndani kiasi cha **milioni 400**, Kazi imehusisha uchimbaji na ulazaji wa bomba za **inchi 6** na **inchi 8** kwa umbali wa **Kilomita 5.7**," amesema **Mhandisi Dorcas**.

"Utekelezaji wa mradi huu kwa makadirio yetu tuliyojiwekea ni kukamilika mwishoni mwa mwezi **Oktoba 2026**, na kwa sasa tumebakiza eneo dogo zaidi kulaza bomba ili wananchi waanze kupata maji," amesema **Mhandisi Dorcas**

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtaa wa **Kimara B Ndugu Beruki Kikwala** ameipongeza **DAWASA** kwa hatua iliyochukua kutatua kero ya wakazi wa mtaa huo ambapo kwa sasa wanatarajia kuwa na uhakika wa huduma tofauti na ilivyokuwa kabla.

"Kwa niaba ya wananchi wenzangu wa King'ongo tunaipongeza **DAWASA** kwa kazi kubwa wanayoifanya, maana tulikuwa hatuna imani kama ipo siku tungepata majisafi, tunaona wapo katika hatua za mwisho hivyo mimi na wananchi wenzangu tunaimani mradi unaenda kukamilika hivi karibuni" amesema **Kikwala**.